

Taarifa kwa
Wanafamilia:

Fahamu kuhusu Hatari
na Hatua za Kudhibiti
Maambukizi ili
Kumkinga Mpendwa
Wako **Aliyelazwa**
Hospitalini



Jinsi Unavyoweza Kumkinga Mpendwa Wako

Maambukizi ni magonjwa ambayo yanababishwa na viini kama vile bakteria, kuvu, vimelea na virusi. Kuwaambukiza wagonjwa viini hivi kunaweza kufanya kuva vigumu kwa mgonjwa kupona na kuenda nyumbani. Ikiwa unamtembelea rafiki au mpPENDWA wako, unahitaji kuchukua hatua za kuzuia kusambaza viini.

Njia bora ya **kukoma kusambaza viini** ni:

- **Kunawa mikono** mara kwa mara
- **Kukaa nyumbani ukiwa mgonjwa**- Usiende hospitalini ikiwa wewe ni mgonjwa au umekuwa na dalili yoyote ya ugonjwa ikiwa ni pamoja na lakini si tu kichefuchefu, kutapika, kuendesha, homa (au kuhisi joto), kikohozi kisichodhibitika, au vipele
- Ikiwa mtu unayemtembelea yuko kwenye "Hadhari za Kujitenga," zungumza na muuguzi kabla ya kuingia chumbani ili ujue hatua utakazohitajika kufuata, kama vile kuvala barakoa au mavazi mengine ya kujikinga.

Fahamu kuhusu Hatari Kwa Sababu

Mikono ni njia maarufu sana ya kusambaza virusi. **Usafi wa mikono ni moja ya njia muhimu zaidi ambazo familia na marafiki wanaweza kutumia kukomesha msambao wa viini na maambukizi.** Sabuni na kieuzi cha mikono katika vyumba vya wagonjwa ni vya kutumiwa na **kila mtu!**

- **Nawa au angamiza viini kwenye mikono unapoingia na kuondoka chumbani.** Wakumbushe wahudumu wa afya kufanya vivyo hivyo kabla ya kuwatunza wapendwa wako.
- Wageni mara nyingi hutaka kushika mikono au kuwakumbatia au kuwabusu wanafamilia wao ili kuwapa faraja. Ingawa vitendo hivi vinaonyesha upendo na urafiki, pia vinaweza kuchangia kusambaza viini. Wageni wanapaswa **kuwa waangalifu wanapomkumbatia mgonjwa ili kuhakikisha kuwa mikono, midomo, au mavazi yao hayagusi eneo ambalo mgonjwa yuko kwenye hatari ya maambukizi.**
 - Vifaa vya matibabu kama vile IV, bomba la kulishia, au uwazi ndani ya mwili kama vile kidonda au sehemu ya upasuaji hutoa fursa kwa viini kuingia kwenye mwili au mkondo wa damu wa mgonjwa na kusababisha maambukizi.

Sehemu za juu zinaweza kupata uchafu kwa urahisi katika vituo vya huduma za afya kutoka kwa viini hewani au kwenye damu na majimaji ya mwili. Mara nyingi, viini hivi ni vidogo sana kuweza kuona kwa jicho la kawaida. Ili kuepuka kusambaza viini sehemu za juu, wageni na wagonjwa wanapaswa:

- **Kunawa au kutumia kieuzi cha mikono** kabla na baada ya kugusa vifaa vya matibabu, zana, reli za vitanda, sehemu za juu, uwazi ndani ya mwili, kabla na baada ya kula na baada ya kutoka msalani.
- **Kupunguza mikusanyiko ya vitu** na kuweka vitu vya mgonjwa mbali na sakafu na vyombo vya taka.
- **Kuruhusu watu kusafisha chumba cha hospitali**, hata wakati mtu hahisi kufanya hivyo. Kusafisha na kuangamiza viini kwenye chumba husaidia kulinda kila mtu kwa kupunguza hatari ya kupata maambukizi—usiseme, "rudi baadaye."